# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz


## Taarifa kwa Umma: Matukio ya Ukiukwaji wa Haki za Kiraia na Kisiasa

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimeendelea na ufuatiliaji wa haki za binadamu kwa lengo la kuhakikisha misingi ya haki za binadamu na misingi ya kidemokrasia inazingatiwa nchini Tanzania. Kwa kipindi cha hivi karibuni Kituo kimebaini ukiukwaji wa haki za binadamu na misingi ya kidemokrasia hususani Haki za Kiraia na Kisiasa kinyume na ilivyoidhinishwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa 1966 na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977. **Mchakato wa kidemokrasia**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimefuatilia kwa karibu taratibu za awali katika uchaguzi mdogo wa madiwani uliopangwa kufanyika katika kata 77 sambamba na uchaguzi wa ubunge katika jimbo la Buyungu mkoani Kigoma. Katika kipindi cha hivi karibuni, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeshuhudia kuwepo kwa matukio mbalimbali yanayoathiri haki za binadamu hususani mchakato wa kidemokrasia kwa wananchi kushiriki katika uchaguzi ulio huru na haki kama inavyoainishwa katika Mikataba ya Kimataifa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Sheria mbalimbali za nchi. Kituo kimebaini ukiukwaji wa *Ibara ya 25* ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa na Kiraia wa 1966 pamoja na Ibara ya 5 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayoweka haki ya ushiriki wa shughuli za kisasa kwa kuainisha haki ya kupiga kura.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimepata taarifa za kitendo cha wananchi kujichukulia sheria mikononi kilichojitokeza katika Kata ya Tunduma, Halmashauri ya Wilaya ya Mji wa Tunduma ambapo wananchi walichoma moto nyumba ya mgombea aliyehama kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleao (CHADEMA) na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinakemea kitendo hicho ambacho ni kinymecha sheria kwani kila mtu ana haki ya kuchagua kujiunga na chama chochote bila kujali hisia za wengine, hata hivyo kitendo cha kutishia maisha yake ni tishio kwa haki ya msingi ya kuishi.

Kwa upande mwingine kumekuwepo na hali ya sintofahamu miongoni mwa wananchi katika kata zipatazo 30 ambapo wananchi wamepokwa haki yao ya ushiriki katika uchaguzi mdogo baada ya baadhi ya wagombea hususani wa vyama vya upinzani kuenguliwa katika mchakato wa uteuzi wa wagombea kwa sababu mbalimbali zikiwemo tuhuma za kutokidhi vigezo vya kiufundi kisheria kama kutokujua kusoma na kuandika pamoja na vigezo vya kutokua raia.

Kwa mujibu wa *Ibara ya 13(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977;*


**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member

*''Ni marufuku kwa mtu yoyote kubaguliwa na mtu au* ***mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote*** *au katika utekelezaji wa kazi au* ***shughuli yoyote ya mamlaka ya nchi.''*** Hivyo, kuenguliwa kwa idadi kubwa ya wagombea hususani wa vyama vya upinzani ni kiashiria cha ukiukwaji wa *Ibara ya 13(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.*

Ikumbukwe kwamba, nchi yetu ni nchi ya kidemokrasia na inayofuata misingi ya mfumo wa vyama vingi tangu mwaka 1992, Sheria ya Vyama vya Siasa imeweka mfumo wa vyama vingi ni vyema usawa ukazingatiwa pasipo ubaguzi wa aina yoyote ile ili kuweka mazingira ya uchaguzi kuwa huru na yenye uwazi.

**Hali ya Haki za Kiraia na kisiasa**

Pamoja na matukio ya ukiukwaji wa misingi ya kidemokrasia, Kituo kimebaini mienendo inayopelekea uvunjifu wa haki za binadamu hususani haki ya mtuhumiwa kupata dhamana. Kwa mujibu wa ibara 13(6)b ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 pamoja na maamuzi ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania katika shauri la madai ya ***Rufaa Na. 65 ya 2016 ikimhusisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Jeremia Mtobesya,*** dhamana kwa mtuhumiwa ni haki ya kikatiba na matakwa ya misingi ya haki za binadamu. Pia ikumbukwe pia katiba yetu inatoa haki ya dhamana ya kutokuwa na hatia. Ibara ya 13(6)(b) inasema

*Ni marufuku kwa mtu anayeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo.* Kitendo cha kukataza watu kuwekewa dhamana kwa makosa yanayowakabili mahakamani na sawa wa kuwahesabia hatia tayari.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeshtushwa na mfululizo wa vitendo na kauli zinazotolewa na viongozi wa Serikali zinazokiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 pamoja na sheria mbalimbali za nchi. Kupitia barua ya Tarehe 16 Julai, 2018 kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji wa Tunduma, Songwe yenye Kumb: TTC/01/89/49 kwenda kwa watendaji wa kata wote kuzuia watendaji kutotoa barua za kuwawekea dhamana wanaokabiliwa na mashauri polisi na mahakamani, agizo hilo linakinza haki za binadamu.

Pia Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapinga vikali Kauli ya Mh. Kangi Lugola Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliyoitoa mnamo Julai 21, 2018 katika mkutano wake na waandishi wa habari kwa askari wa usalama barabarani kutomfikisha mshtakiwa Mahakamani kwa kosa la usalama barabarani atakayesababisha ajali kwa ubovu wa gari bila kumlaza mtu huyo mahabusu. Ni wazi kuwa, kauli hii inakiuka miongozo ya kikatiba inayoweka misingi ya dhamana pamoja na dhana ya kutokuwa na hatia mpaka pale itakapothibitika ***( Presumption of Innocence)*** kama ilivyoainishwa katika ibara 13 (6) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Kitendo hiki kinaweka mazingira magumu kwa mtuhumiwa kufikia haki ya kupata dhamana kama haki yake ya kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 13 (6) (b) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, na kupelekea kucheleweshwa kwa haki au kukosa kabisa haki ya dhamana kwani haki iliyocheleweshwa ni haki iliyonyimwa. Pia sheria ya mwenendo wa makosa

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member

ya jinai (Criminal Proceduire Act) sura ya 20 ya sheria za Tanzania imeweka bayana taratibu za kuchukua dhidi ya watu wanatuhumiwa kwa makosa mbalimbali. Kwenda kinyume na utaratibu wa kisheria ni kupuuza utawala wa sheria na pia inaweza kuadhri shauri lote la jinai kama litafika mahakamani maana mtuhumiwa anaweza akawa ametenda kosa kweli lakini mahakama ikamwachia huku kwa vile taratibu za kisheria hazikufuatwa toka mwanzoni. Kituo hakitosita kumfikisha kiongozi yoyote Mahakamani atakaetoa maagizo yanayokiuka misingi ya Mikataba ya kimataifa inayolinda haki za binadamu, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 pamoja na sheria za nchi.

Kufuatia hali hiyo, Kituo cha Sheia na haki za Binadamu kinaisihi Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuzingatia isingi a kidemokrasia na kutenda haki katika kusimamia chaguzi nchini.

Mwisho, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatoa rai kwa Mamlaka za Serikali pamoja na wananchi kwa ujumla kuheshimu misingi ya kikatiba pamoja na kisheria katika kutekeleza majukumu yake.

**Imetolewa Julai 23, 2018 na,**

**Bi. Anna Henga (Wakili)**
**Mkurugenzi Mtendaji**

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member